

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Dodoma
Anwani ya Simu REGCOM
Simu Nambari: 2324343/2324384
E-Mail No. ras@dodoma.go.tz
Fax No. 255 026 2320046



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P 914,
Dodoma.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Jordan Rugimbana amewapa siku kumi (10) kuanzia leo, wafanyabiashara wote wa mafuta Mkoani Dodoma, kuhakikisha wamefunga mashine za kieletroniki za kuuzia mafuta kwenye vituo vyao zinazoiwezesha Serikali kukusanya kodi na endapo watakaidi watafungiwa vituo vyao vya mafuta.

Agizo hilo limetolewa wakati wa kikao alichokiitisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ofisini kwake Julai 15, 2017 kilichohudhuriwa na Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Dodoma Ndugu Thomas Masese na viongozi wa chama cha Wafanyabiashara wa mafuta Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Rugimbana aliwataka wamiliki wote wa vituo kuhakikisha ndani ya Siku hizo kumi (10) wale waliokwisha nunua mashine hizo za kieletroniki na sasa wanasubiri kufungiwa kwenye vituo vyao, kukamilisha ufungaji wa mashine na wale waliokwisha lipia mashine hizo kwa mawakala wa TRA na wanasubiri kuletewa mashine hizo, ameahidi kwa kushirikiana na TRA wataweka msukumo mashine hizo zipatikane kwa haraka na kufungwa kwenye vituo vya mafuta.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Dodoma Ndugu Thomas Masese amesema wafanyabiashara wengi wa Mkoa wa Dodoma wana ushirikiano na mwamko mzuri wa kulipa kodi husani kwa kutumia mashine hizo za kielektroniki na kuwa vituo vingi Mkoani Dodoma vimeshafunga mashine za kielektroniki na vichache vinasubiri kuletewa mashine hizo na mawakala wa usambazaji wa TRA.

Ameongeza kuwa ushirikiano na mwamko wa kulipa kodi kwa wafanyabiashara wa Dodoma, umechangia kuiwezesha TRA kuvuka lengo katika kukusanya kodi ambapo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2017 walipangiwa kukusanya shilingi Bilioni 47 lakini makusanyo halisi yalivuka kufikia shilingi Bilioni 52.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa mafuta Kanda ya kati Ndugu Faustine Mwakalinga alitumia kikao hiko kuishukuru Serikali kwa kutoa muda huo wa siku kumi ili kukamilisha ufungaji wa mashine hizo za kielektroniki kwenye vituo vyote vya kuuzia mafuta.


Jeremia Mwakyoma

Afisa Habari na Uhusiano
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma
Julai 16, 2017